Je Krismasi Ndio Siku Aliyozaliwa Yesu?

(Is Christmas The Birthday of Jesus?)

Na

Ellis P. Forsman

Je Krismasi Ndio Siku Aliyozaliwa Yesu?

(Is Christmas The Birthday of Jesus?)

Na

Ellis P. Forsman

Desemba 16, 2017

Je Krismasi Ndio Siku Aliyozaliwa Yesu?

Maana watu wengi ulimwenguni kote, msimu wa Krismasi ndio mwaka wenye furaha na shughuli nying kwao. Mamilioni ya waumini katika Kristo husheherekea Disemba 25th kama sikukuu muhimu ya kidini kwa sababu wanaamini kuwa inaonyesha tarehe ambayo Yesu alizaliwa. Lakini Disemba 25th yaweza kuwa ndio siku aliyozaliwa Kristo? Wafanya biashara mara nyingi huchukua nafasi hiyo kutoa zawadi katika msimu huu ili kutengeneza faida ya ziada. Baadhi ya watu wa dini huandamana wakati huu wa "biarashara" ya Krismasi kwa sababu wanahisi kwamba ni safi, siku ya mapumziko hutengenezwa nayo. Maandamano yao mara nyingi huwa na kauli mbiu kama "Mrudishe Kristo katika Krismasi." Watu wachache, hataivyo, ukijumuisha waumini wengi katika Kristo, wanafahamu ukweli kwamba Biblia imenyamaza kuhusu sikukuu yoyote mhumu ya kumbukumbu ya kuzaliwa Kristo. Historia inaonyesha kwamba Disemba 25th ilifanywa kuwa maarufu kama tarehe ya Krismasi, siyo kwamba Kristo alizaliwa katika siku hiyo, lakini kwa sababu ilikuwa ni siku maarufu katika sherehe za dini ya kipagani kama siku ya kuzaliwa jua. Lakini Disemba 25th yaweza kuwa siku ya kuzaliwa Kristo?

Biblia haitupatii tarehe ya siku ya kuzaliwa Yesu! Iwe alizaliwa Disemba au July au mwezi mwingine katika mwaka haijaelezwa katika Maandiko. Wanazuoni wanakiri kwamba hawajui tarehe halisi ya kuzaliwa Kristo. Kwa zaidi ya miaka 300 ikikaribia na kufungwa kwa Agano Jipya, Krismasi iliadhimishwa katika tarehe tofauti. Katika 354, askofu wa Rumi aliamuru kwamba Disemba 25th iwe sikukuu ya mapagani kwa kumheshimu mungu, sayari ya Saturn, inapaswa kuangaliwa na Wakristo katika kuadhimisha siku ya kuzaliwa Kristo. Hataivyo, katika Mashariki, tarehe hii haikukubaliwa; na kwa karne zote Januari 6th ilisheherekewa kama siku ya kuzaliwa Yesu, hasa katika nchi ya Misri. Baadhi ya matawi ya kanisa la Orthodox la Mashariki, hata leo, wanaisheherekea Januari 6th kama Siku ya Krismasi.

Inavutia kujua pia kwamba maadhimisho mengi yanayounganishwa na Krismasi yalikuwa na vyanzo vyao katika upagani, siyo katika Biblia. Mengi yao yalitoka katika Ukatholiki pia. Kwa mfano, jina "Krismasi" lenyewe linatokana na "Kristo" "Masi" inaongelea ibada ya Kanisa la Roman Catholiki. Mti wa Krismasi ulitoka katika nchi za Scandinavia. Wapani waliopo katika sehemu hiyo ya dunia waliabu miti kabla hawajawa waamini katika Kristo. Mapambo ya vimulimuli na mauwa ulitokana na kuhani wa zamani wa Celtic, aliyeitwa Druids, aliyetumia maapambo na vimulimuli kama kifurahisho dhidi ya pepo wabaya. Kuchomwa kwa magogo ya kusheherekea Krismasi, ambayo ni desturi katika nchi nyingi, ulitoka kwa watu wa zamani wenye pua waliochoma

magogo mara moja kwa mwaka katika kumheshimu Thor, mungu wa Radi. Kuna mifano mengine mingi ya wapagani kuvutiwa na desturi ya Krismasi ambayo inaweza kupatikana katika vitabu vya encyclopedia au katika mtandao.

Hataivyo, mchanganuzi makini wa Maandiko, anaonyesha wazi kwamba Disemba 25th isingeweza kuwa siku aliyozaliwa Kristo. Hapa kuna sababu mbili za msingi:

Kwanza, tunafahamu kwamba mashemasi walikuwa katika mashamba wakiangalia makundi yao wakati wa kuzaliwa Yesu (Luka 2: 7-8) "*Akamzaa mwanawe kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni. Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku." Wachungaji hawakuwa makondeni wakati wa Disemba. Kulingana na "Kusheherekea*": Kitabu chote cha sikukuu za Kiamerika, kitabu cha Luka "kinapendekeza kwamba yawezekana Yesu alizaliwa katika majira ya joto au mapema katika vuli. Kwa vile Disemba kuna baridi na mvua katika Yudea, ni dhahiri kwamba wachungaji walipaswa kutafta sehemu ya kupumzika kwa ajili ya wanyama wao usiku." (uk. 309). Pia, kutoka katika "Hali ya hewa na mafira katika Israeli, Sayansi ya Israeli na muongozo wa Teknolojia = "Israeli ipo kati ya viwango 29-33 kaskazini kwa ikueta, ambayo uhesabika kama ukanda wa tropic, kati ya uwanda wa joto na ukanda wa tropic. Sehemu ya kaskazini na puani ya Israeli inaonyesha tabia ya hali ya hewa ya Meditereniani kwa kiwango cha joto na ukavu na wakati wa mvua za vuli. Ambapo sehemu za kusini na mashariki ya Israeli inahesabika kuwa ni kavu sana.

Vile vile, "*mtafsiri wa Komentary ya Ujazo Mmoja"* anasema kifungu hiki kinapingana "dhidi ya kuzaliwa [kwa Kristo] ikitokea Disemba 25th kwa vile hali ya hewa isingeruhusu" wachungaji wakiangalia mifugo yao makondeni usiku.

Pili, wazazi wa Yesu walikuja Bethlehemu kujiandikisha katika Sensa ya Warumi (Luka 2:1-4), "*Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio alipokuwa liwali wa Shamu. Watu wote wakaenda kuandikwa kila mtu mjini kwao. Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi,*" Uandikishaji huo haukutokea wakati wa baridi, wakati hali ya joto iliposhuka hadi kuganda na barabara zilikuwa katika hali mbaya ingekuwa na kushindana mwenyewe.

Ikitoa ugumu na hamu ya kuwaleta mapagani katika Ukristo, "*…ukweli mhimu ninayokutaka uingie wazi katika kichwa chako ni*

kwamba kutengenezwa kwa tarehe kama Disemba 25th ilikuwa inahusiana na mapagani" ("*William Walsh, hadithi ya Santa Klaus", 1970, uk. 62*).

Kama Yesu Kristo hakuzaliwa Disemba 25th, je Biblia inaonyesha ni lini alizaliwa? Biblia inaonyesha kuanguka kwa mwaka kama ndiyo wakati aliyozaliwa Yesu kulingana na dhana na kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.

Kwa vile Elizabeth (mama yake Yohana) alikuwa katika mwezi wake wa sita ya mimba wakati ambapo Yesu alitungwa (Luka 1: 24-36), "*Hata baada ya siku zile mkewe Elizabeti alichukua mimba akatawa miezi mitano, akisema, hivi ndivyo alivyonitendea Bwana katika siku zile alizoangalia ili kuniondolea aibu yangu mbele ya watu. Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu. Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe. Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia usiogope Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu ataitwa Mwana wa aliyejuu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya YAkobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho. Mariamu akamwambia malaika, litakuwaje neno hili maana sijui mume? Malaika akajibu akamwambia Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hichokitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu. Tena tazama jamaa yako Elisabeti naye amechukua mimba ya mtoto mwanamume katika uzee wake; na mwezi huu ni wa sita kwake yeye aliyeitwa tasa;*" tunaweza kukadiria wakati wa mwaka wa Yesu alipozaliwa kama tunafahamu lini Yohana alipozaliwa. Baba yake Yohana , Zakaria, alikuwa kuhani akifanya kazi katika hekalu Yerusalemu wakati wa zamu ya Abiya (Luka 1:5), "*Zamani za Herode, mfalme wa Uyahudi, palikuwa na kuhani mmoja jina lake Zakaria, wa zamu ya Abiya na mkewe alikuwa mmoja wapo wa uzao wa Haruni, jina lake Elisabeti.*" Mahesabu ya kihistoria inaonyesha zamu hii ya utendaji inaingia katika mwezi wa June 13 -19 katika mwaka huo (Biblia Saidizi, 1974, appendix 179, uk. 200).

Ilikuwa ni wakati huu wakati wa huduma ya hekalu kwamba Zakaria alijifunza kwamba yeye na mkewe Elisabeti, wangekuwa na mtoto (Luka 1: 8-13), "*Basi ikawa alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele za Mungu, kama ilivyokuwa desturi ya ukuhani, kura ilimwangukia kuingia katika hekalu la Bwana ili kufukiza uvumba. Na*

makutano yote ya watu walikuwa akisali nje saa ya kufukiza uvumba. Akatokewa na malaika wa Bwana amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia. Zakaria alipomwona alifadhaika, hofu ikamwingia. Lakini yule malaika akamwambia, usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume na jina lake utamwita Yohana." Alipomaliza huduma yake akasafiri kuelekea nyumbani, Elisabeti akapata ujauzito (Luka 1:23-24). "*Ikawa siku za huduma yake zilipokuwa zimetimia akaenda nyumbani kwake. Hata baada ya siku zile mkewe Elisabeti alichukua mimba akatawa miezi mitano akisema,*" Tuchukulie kwamba mimba ya Yohana ilitungwa karibia mwishoni mwa mwezi Juni, jumlisha miezi tisa inatuleta karibia mwisho wa mwezi Machi kama ilivyo wakati alipozaliwa Yohana. Ukijumlisha miezi sita nyingine (tofauti katika umri kati ya Yohana na Yesu (Luka 1: 35- 36), "*Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliyejuu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu Mwana wa Mungu. Tena tazama jamaa yako Elisabeti amechukua mimba ya mtoto Mwanamume katika uzee wake na mwezi huu ni wa sita kwake yeye aliyeitwa tasa;*" Inatuleta mwishoni mwa Septemba inavyofanana na wakati Yesu alipozaliwa.

Hata kama ni vigumu kutambua mara ya kwanza mtu yeyote anaposheherekea Disemba 25th kama siku ya Krismasi, wanahistoria wako katika makubaliano ya pamoja kwamba ilikuwa takriban karne ya nne. Hii inashangaza kwamba ni tarehe iliyochelewa. Krismasi haikusheherekewa Rumi, mji mkuu wa utawala wa Kirumi, hadi takriban mika 300 baada ya kifo cha Kristo. Mwanzo wake haiwezi kuangaliwa nyuma aidha katika mafundisho au vitendo vya Wakristo wa kwanza.

Biblia inatupatia sehemu mbili za kuzaliwa kwa Yesu. Zinapatikana katika Mathayo 1 na 2 na Luka 2. Hakuna tarehe inayoonyeshwa. Hakuna agizo linalotolewa ya kuzaliwa kwa Bwana wetu kwamba iweze kusheherekewa kwa njia yoyote ile. Hakuna mfano unaopatikana katika Agano Jipya ya sherehe yoyote ya kuzaliwa Kristo. Isipokuwa msisitizo wa Agano Jipya upo katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo. Kifo chake kiliwezesha msamaha wa dhambi zetu. ufufuo wake unafanya ushindi wetu dhidi ya mauti iwezekane. Meza ya Bwana ni kutangaza mauti yake mpaka atakapokuja (1 Kor. 11:26). Siku pekee iliyotengwa kwa ajili ya huduma ya kidini katika Agano Jipya ni siku ya Bwana, Juma pili, siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:2; Ufu. 1:10).

Tabia ya Mkristo inapaswa kuwaje dhidi ya Krismasi? Je tunapaswa kuisheherekea kama siku aliyozaliwa Kristo? Hakika hapana! Kufanya hivyo ni kutokuwa na mamlaka ya maandiko. Je tunapaswa kusheherekea sikukuu ya Krismasi kwa namna yoyote ile? Katika

mawazo ya huyu mwandishi, hakuna ubaya wa kufurahi katika sikukuu ya Krismasi, sawa na mtu anavyoweza kufurahia siku nyingine yoyote katika mwaka. Kama mtu anapenda kuwa na chakula kikubwa na kuwa pamoja na familia na marafiki, hakika hakuna ubaya katika hili. Lakini kuheshimu Disemba 25th kama siku aliyozaliwa Kristo, na hivyo kuifanya kuwa sikukuu maalum, ni kuongea iliponyamaza maandiko na kufuata desturi ya wanadamu kuliko Neno la Mungu.